# UCHAGUZI
## Jarida

Jarida la Tume ya Taifa ya Uchaguzi    Toleo Na. 19    Januari, 2024




# Maandalizi uboreshaji wa Daftari yapo kwenye hatua za mwisho


02 TUME YATANGAZA UCHAGUZI MDOGO KATA 23 ZA TANZANIA BARA

09 NEC YATEUA MADIWANI WANAWAKE WATANO WA VITI MAALUM

Ifahamu Tume

# Njia za Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikitekeleza mkakati wa kutoa Elimu ya Mpiga Kura endelevu kwa kutumia njia zifuatazo;

**(I)mikusanyiko rasmi ya watu:** Tume inatumia maonyesho mbalimbali kama vile Sabasaba, Nanenane, Mikutano ya Serikali za Mitaa (ALAT) na wiki ya vijana kwa kutoa Elimu ya mpiga Kura ana kwa ana au kuwapatia vijitabu na vipeperushi vyenye kuonesha hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi;

**(ii)mikutano na wadau:** Tume hufanya mikutano na wadau mbalimbali ikiwa ni njia ya kutoa elimu. Aidha, imekuwa ikiandaa mikutano katika shule mbalimbali za sekondari kwa lengo la kuwaelimisha wapiga kura watarajiwa kuhusu shughuli za Tume na michakato ya Uchaguzi ili kuwahamasisha kushiriki katika Uchaguzi;

**(iii)vipindi vya Redio na Televisheni:** Tume inaandaa na kutekeleza programu ya kushiriki katika vipindi mbalimbali vya redio na runinga ili kuweza kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria,kanuni na maelekezo.

**(iv)makala za magazeti:** Tume huandaa makala zinazohusu masuala ya Uchaguzi na kuzichapisha katika magazeti mbalimbali nchini kwa lengo la kutoa habari na kuelimisha umma kuhusu Sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji Uchaguzi.

**(v)mitandao ya Kijamii:** Tume imekuwa ikitumia mitandao ya kijamii katika kutoa habari za kuelimisha na kuhabarisha.

**(vi)vijitabu, vijarida na vipeperushi:** Tume imekuwa ikiandaa vijitabu na vijarida mbalimbali ambavyo huvigawa kwa wananchi bure.

**(vii)sanaa:** Tume imekuwa ikitumia nyimbo na michezo ya kuigiza ambayo huandaliwa kwa kushirikiana na wasanii mbalimbali. Nyimbo hizo na michezo hutumika katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

**(viii)gari la Matangazo:** Tume hutumia gari lake la matangazo ambalo hupita katika maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko ya watu kama vile stendi, sokoni, minadani na shuleni ili kutoa Elimu ya Mpiga kura ana kwa ana.

# TUME YATANGAZA UCHAGUZI MDOGO KATA 23 ZA TANZANIA BARA



*Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Mhe. Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele (katikati) akiongoza kikao cha Tume jijini Dodoma tarehe 15 Februari, 2024 ambapo pamoja na mambo mengine kilitangaza uchaguzi mdogo wa kata 23 za Tanzania Bara utakaofanyika tarehe 20 Machi, 2024. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Tume, Mhe. Jaji (Rufaa) Mstaafu, Mbarouk Salim Mbarouk na kulia ni Katibu wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Kailima, R. K.*

**Na Mwandishi Wetu**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imetangaza uchaguzi mdogo wa madiwani kwenye kata 23 za Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Kailima, R. K jijini Dodoma tarehe 15 Februari, 2023 uchaguzi huo utafanyika tarehe 20 Machi, 2024.

“Fomu za uteuzi zitatolewa kuanzia tarehe 27 Februari, 2024 hadi tarehe 04 Machi, 2024, uteuzi wa wagombea utafanyika tarehe 04 Machi, 2024 na kampeni za uchaguzi zitafanyika kuanzia tarehe 05 hadi 19 Machi, 2024,” imesema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo imeanisha kuwa uchaguzi huo umetangazwa kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, akiitaarifu Tume kuhusu uwepo wa nafasi wazi za madiwani katika kata 23 za Tanzania Bara.
Taarifa hiyo imesema kuwa Waziri ametoa taarifa hiyo kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

“Tume inatumia nafasi hii kuvikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na maelekezo ya Tume katika kipindi cha uchaguzi huu mdogo,” imesema taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kata zitakazofanya uchaguzi huo mdogo ni Kimbiji (Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni), Kasingirima (Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji), Ndevelwa (Halmashauri ya Manispaa ya Tabora), Msangani (Halmashauri ya Mji Kibaha), Fukayosi (Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo), Mlanzi (Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti), Utiri (Halmashauri ya Mji Mbinga) na Mbingamhalule (Halmashauri ya Wilaya ya Songea).

Nyingine ni Isebya (Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe), Kibata (Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa), Mshikamano (Halmashauri ya Manispaa ya Musoma), Busegwe (Halmashauri ya Wilaya ya Butiama), Nkokwa (Halmashauri ya Wilaya ya Kyela), Kamwene (Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba), Chipuputa (Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu), Buzilasoga (Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema), Mhande (Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba), Kabwe (Halmashauri ya Nkasi), Bukundi (Halmashauri ya Wilaya ya Meatu) Mkuzi (Halmashauri ya Wilaya ya Muheza) na Boma, Mtimbwani na Mayomboni (Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga).



# TAHARIRI



*Maafisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakitoa Elimu ya Mpiga Kura kwa wananchi waliotembelea banda la Tume kwenye maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya miaka 60 yaliyofanyika katika viwanja vya Nyamanzi (Fumba Town).*

## Wananchi, Tumieni Fursa ya Maonesho Kupata Elimu ya Mpiga Kura

Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yaliyofanyika katika viwanja vya Nyamanzi (Fumba Town) kuanzia tarehe 7 hadi 19 Januari 2023 na maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika kati ya tarehe 24 hadi 30 Januari, 2024 katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma yalitumiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa ajili ya kutoa elimu ya mpiga kura kwa wananchi kwa njia ya ana kwa ana.

Maonesho ya Zanzibar yamefanyika ili kuenzi Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ambayo yametimiza miaka 60, wakati maonesho ya Dodoma ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Sheria ambapo Tume iliitumia ipasavyo mikusanyiko hiyo kutoa Elimu ya Mpiga Kura.

Kupitia mikusanyiko hiyo wananchi walipewa elimu ya mpiga kura na Maafisa wa Tume kwa njia ya ana kwa ana, na kupatiwa vipeperushi na vijitabu mbalimbali vinavyoelezea majukumu ya Tume. Elimu ya mpiga kura ni muhimu kwani huwajengea uelewa wananchi kuhusu haki na wajibu wao wa kushiriki uchaguzi wakiwa na taarifa kamili na sahihi juu ya mchakato wa Uchaguzi.

Mathalani, katika maonesho ya Zanzibar, Maafisa wa Tume walipata fursa ya kutoa ufafanuzi na kuwaeleza wakazi wa Zanzibar kuhusu utaratibu unaotumika kuwaandikisha wapiga kura wanaoishi visiwani humo ambao hawakidhi vigezo vya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ili waweze kushiriki katika upigaji kura wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kadhalika wananchi nao walipata fursa ya kuelewa kwa undani hatua za kujiandikisha kama wapiga kura na umuhimu wa kushiriki katika zoezi la uchaguzi. Lakini pia walipata fursa ya kuuliza maswali mbalimbali na kujibiwa papohapo.

Kwa kutambua umuhimu wa elimu ya mpiga kura kuwafikia wadau mbalimbali wa uchaguzi hususani wapiga kura, tunapenda kutoa wito kwa wananchi kuendelea na moyo wa kutembelea mabanda ya Tume na kupata elimu ya mpiga kura kupitia maonesho mbalimbali ambayo Tume itashiriki.

Vile vile, tunatoa wito kwa wananchi kutumia fursa mbalimbali za kupata elimu ya mpiga kura ikiwemo ile inayotolewa kupitia mikutano ya Tume na wadau, machapisho kwenye tovuti na kurasa za mitandao ya kijamii ya Tume.

Pia tunawaasa wananchi kutumia fursa ya kupata elimu ya mpiga kura kwa njia ya vipindi vya redio na televisheni vinavyoandaliwa na Tume kwa lengo la kuwaelimisha wananchi kuhusu majukumu ya Tume.

# MAANDALIZI UBORESHAJI WA DAFTARI YAPO KWENYE HATUA ZA MWISHO



*Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele akifanya mahojiano na waandishi wa habari visiwani Zanzibar baada ya kutembelea maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya miaka 60 yaliyofanyika katika viwanja vya Nyamanzi (Fumba Town).*

**Na Mwandishi Wetu**

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji (Rufaa), Mhe. Jacobs Mwambegele amesema Tume inaendelea vizuri na maandalizi ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na itawajulisha wananchi hivi karibuni kuhusu tarehe ya kuanza kwa zoezi hilo.

Mhe. Mwambegele ameyasema hayo hivi karibuni muda mfupi baada ya kutembelea banda la Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa mahojiano na waandishi wa habari kwenye Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa ikiwa ni sehemu ya Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya miaka 60 yaliyofanyika katika viwanja vya Nyamanzi (Fumba Town).

"Tume ya Taifa ya Uchaguzi itawatangazia wananchi tarehe ya kuanza kwa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, si muda mrefu kutoka sasa. Tayari tumeshafanya uboreshaji wa majaribio wa Daftari kujaribu vifaa vyetu, majaribio yameenda vizuri na tutawajulisha Watanzania wakati muafaka utakapofika wa kuanza kwa zoezi hilo," amesema Jaji Mwambegele.

Kuhusu sifa ambazo mwananchi atapaswa kuwa nazo ili aweze kujiandikisha kuwa mpiga kura, Mwenyekiti wa Tume amesema kuwa pamoja na sifa nyingine, sifa kuu za kuweza kuandikishwa kwenye Daftari ni uraia na kutimiza umri wa kupiga kura.

"Mtu ili aweze kuandikishwa kuwa mpiga kura anatakiwa awe mtanzania na awe ametimiza umri wa kupiga kura ambao ni miaka 18. Anaweza kuwa na kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA ili kuthibitisha uraia wake," amesema.

Jaji Mwambegele amesema mpiga kura anayeboresha taarifa zake anapaswa kwenda kwenye kituo cha kuandikisha wapiga kura na kadi yake ya mpiga kura ambayo ilitolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

"Tunayo kadi ya mpiga kura, mpiga kura anayehitaji kuboresha taarifa zake anatakiwa kuwa na kadi ya mpiga kura ambayo inatolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi," amesema.

Kuhusu uandikishaji wa wapiga kura Zanzibar, Mhe. Mwambegele amesema kuwa Tume itatumia Daftari la Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kwa ajili ya Uchaguzi kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

"Katiba zote mbili; ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar zinatutaka tufanye kazi kwa kushirikiana na tukiwa hapa Zanzibar tunatumia Daftari la ZEC kwenye uchaguzi," amesema.

Akieleza kuhusu changamoto ya uchukuaji wa alama za vidole (fingerprint) wakati wa uboreshaji wa Daftari na jinsi Tume ilivyojipanga kukabiliana na tatizo endapo litajitokeza, Jaji Mwambegele amesema teknolojia inayotumika kuboresha Daftari inaruhusu njia mbadala kutumika kumpatia mwananchi haki ya kupiga kura hata kama kutakuwa na changamoto ya kuchukua alama zake za vidole.

"Tulipokuwa tunafanya uboreshaji wa majaribio hatujakutana na tatizo hilo, tunaelewa kwamba pale ambapo fingerprint hazisomeki haswa maeneo ya vijijini zipo njia za kufanya ili wananchi wapate haki yao ya kujiandikisha," amesema.

Kuhusu sababu za Tume kufanya maonesho Zanzibar, Jaji Mwambegele amesema "wote mnajua kwamba tulikuwa na sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, sambamba na hilo sisi Tume ya Taifa ya Uchaguzi tumekuja kwenye maonesho haya kwa lengo la kuwaelimisha wananchi, kuhusu majukumu ya Tume," ameongeza kwa kusema:

"Mnajua kwamba Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar zinahitaji Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar zifanye kazi kwa kushirikiana. Kwa hiyo kuweka banda hapa ni katika kuonesha mshikamano huo na

> ***"Katiba zote mbili; ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar zinatutaka tufanye kazi kwa kushirikiana na tukiwa hapa Zanzibar tunatumia Daftari la ZEC kwenye uchaguzi," amesema Jaji (Rufaa) Mwambegele.***

# BUNGE LAPITISHA MISWADA YA UCHAGUZI



*Kutoka Kushoto ni Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe.Jaji (Rufaa) Jacobs C. Mwambegele, Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe.Jaji (Rufaa) (Mst) Mbarouk S.Mbarouk, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, Mhe.Jaji George J.Kazi na Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibat (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi), Mhe.Hamza Hassan walipokuwa wakifuatilia mjadala wa Miswada ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, wabunge na Madiwani ya mwaka 2023 na Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi*

**Na Mwandishi Wetu**

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha miswada miwili inayoihusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo inalenga kuimarisha utawala bora na demokrasia nchini.

Miswada hiyo ni Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa mwaka 2023 na Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023.

Miswada hiyo imejadiliwa katika kikao cha 14 cha Bunge jijini Dodoma kuanzia tarehe 30 Januari hadi tarehe 01 Februari, 2024, na imepitishwa tarehe 02 Februari, 2024.

Kabla ya miswada hiyo kupitishwa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Mhe. Jenista Mhagama amesema kuwa serikali imeridhia mapendekezo ya Wabunge wengi ya kutaka jina la Tume ya Uchaguzi libadilike na kuwa Tume huru ya Uchaguzi.

Amesema kwamba, Serikali haina tatizo na utekelezaji wa maoni ya wadau waliopendekeza uwepo wa neno 'huru' kwenye jina la Tume kwa kuwa msingi wa uhuru huo upo kwenye ibara ya 74(7) na 74(11) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Kwa mujibu wa Ibara ya 74(7) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tume ya Uchaguzi itakuwa ni idara huru inayojitegemea, itafanya maamuzi yake rasmi kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa vikao, na mtendaji wake mkuu atakuwa ni Mkurugenzi wa Uchaguzi ambaye atateuliwa na kufanya kazi kwa mujibu wa masharti ya sheria iliyotungwa na Bunge.

Kadhalika, Ibara ya 74(11) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inafafanua katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali, au maoni ya chama chochote cha siasa.



*Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson akizungumza wakati wa kuhitimisha mjadala wa Sheria zinazohusu Uchaguzi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi Februari 2, 2024 Bungeni jijini Dodoma.*

# TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI YATOA ELIMU YA MPIGA KURA ZANZIBAR



*Mkurugenzi wa Ofisi ya Zanzibar wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Adam Mkina alipotembelea banda la Tume katika maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya miaka 60 yaliyofanyika katika viwanja vya Nyamanzi (Fumba Town).*

**Na Mwandishi Wetu**

BTume ya Taifa ya Uchaguzi katika kuyaenzi Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ambayo yametimiza miaka 60, imeshiriki kutoa elimu ya mpiga kura kwa wakazi wa Zanzibar kupitia maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yaliyofanyika katika viwanja vya Nyamanzi (Fumba Town) kuanzia tarehe 7 hadi 19 Januari 2024.

Akielezea ushiriki wa Tume kwenye maonesho hayo, Mkurugenzi wa Ofisi ya Zanzibar wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Adam Mkina, amesema, Tume imetumia fursa hiyo kutoa elimu ya mpiga kura kwa njia ya ana kwa ana kwa wakazi wa Zanzibar.

Bw. Mkina amewashukuru wananchi hao kwa kujitokeza kwa wingi kwenye maonesho hayo kwa lengo la kupata elimu ya mpiga kura, kutambua majukumu yao kama wapiga kura na kufahamu sheria, kanuni na taratibu zinazohusika katika mchakato wa uchaguzi.

Aidha, Mkurugenzi huyo ametaja baadhi ya mafanikio ya Tume kuwa ni pamoja na kuratibu shughuli za uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na usimamizi wa uchaguzi katika majimbo 50 ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa Bw. Mkina, Tume itaandikisha wapiga kura ambao hawakukidhi vigezo vya kuandikishwa na ZEC lakini wana sifa ya kupiga kura ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vigezo hivyo ni kuwa Mzanzibari mwenye kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Hivyo watanzania wote wanaoishi Zanzibar lakini wamekosa sifa ya Mzanzibar Mkaazi huandikishwa na NEC ili waweze kupiga kura ya Rais wa Jamhuri ya Muungano.

"Tunawapata wananchi wengi kutoka Tanzania Bara ambao huja Zanzibar kwa shughuli za kiuchumi na biashara na Wazanzibar ambao hawajatimiza sifa ya kupata kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi," amesisitiza Bw. Mkina.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ambayo pamoja na mambo mengine inaitaka Tume kusimamia na kuratibu uandikishaji wa Wapiga Kura katika uchaguzi wa Rais, Wabunge katika Jamhuri ya Muungano na Madiwani kwa Tanzania Bara.

Pia Kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Uchaguzi wa Rais na Wabunge, kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya Uchaguzi wa Wabunge.

Aidha, majukumu mengine yaliyowekwa kwa mujibu wa kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ni kutoa Elimu ya Mpiga Kura kwa nchi nzima, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo na kuteua madiwani wanawake wa viti

*Inaendelea Uk.07*

Inatoka Uk.06

maalum.

Pia Ibara 74 (13) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imeelekeza kuwa katika utekelezaji wa madaraka yake, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) itashauriana mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).

NEC na ZEC zimekuwa zikifanya hivyo kila mara kwa kukutana na kufanya vikao vya pamoja kuhusiana na utekelezaji wa majukumu yao.

Mafanikio mengine ni pamoja na upatikanaji wa Jengo la Ofisi ya Zanzibar la Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Kabla ya kuwepo kwa jengo hilo, NEC ilikuwa inategemea miundombinu ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), lakini sasa, ina ofisi yake na imeweza kuboresha utekelezaji wa shughuli za uchaguzi kwa upande wa Zanzibar kwa ufanisi zaidi.

# NEC YAPONGEZWA KWA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA



*Maafisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakitoa Elimu ya Mpiga Kura kwa wananchi waliotembelea banda la Tume kwenye maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya miaka 60 yaliyofanyika katika viwanja vya Nyamanzi (Fumba Town).*

**Na Mwandishi Wetu**

Baadhi ya wananchi waliotembelea Banda la Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sherehe za miaka 60 za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yaliyofanyika katika viwanja vya Nyamanzi (Fumba Town) wameipongeza Tume kwa kushiriki maonesho hayo na kutoa elimu ya mpiga kura kwa njia ya ana kwa ana kwa wakazi wa Zanzibar.

Mmoja wa wananchi waliotembelea banda la Tume wakati wa maonesho hayo yaliyofanyika kuanzia tarehe 7 hadi 19 Januari, 2024, Bw. Salum Pazi amesema miongoni mwa vitu vilivyomfurahisha baada ya kutembelea banda hilo ni kufahamu tofauti ya majukumu kati ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

Amesema elimu ya mpiga kura inayotolewa ni nzuri kwa sababu inawawezesha wananchi kufahamu taratibu za mchakato wa Uchaguzi, ikiwa ni pamoja na kuelewa wajibu wao na umuhimu wao wa kushiriki kikamilifu mchakato wa uchaguzi.

Mwananchi mwingine ambaye amepata fursa ya kutoa maoni yake baada ya kutembelea banda la Tume ni Bi. Khadija Hassan Mkaja (mwenye ulemavu wa kusikia) ambaye ameitaka Tume kuhakikisha kuwa elimu ya mpiga kura inawafikia kwasababu watu wenye uziwi wamekuwa wakipata changamoto ya kupata habari mbalimbali zikiwemo habari zinazohusu mchakato wa uchaguzi katika visiwa vya Zanzibar.

Kwa upande wake, Bw. Omar Salim Mbarouk amesema kitendo cha elimu ya mpiga kura kutolewa kila baada ya miaka mitano wakati wa uchaguzi mkuu kinachangia wananchi walio na uelewa mdogo kuhusu mchakato wa uchaguzi kutoona umuhimu wa kushiriki kikamilifu katika zoezi la kujiandikisha na kupiga kura.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imetumia fursa hiyo kutoa elimu ya mpiga kura kwa njia ya ana kwa ana kwa wakazi wa Zanzibar ambapo wananchi waliotembelea Banda la Tume walipata fursa ya kupewa elimu ya

Inaendelea Uk.08

Inatoka Uk.07

mpiga kura, kutambua majukumu yao kama wapiga kura na kufahamu sheria, kanuni na taratibu zinazohusika katika mchakato wa uchaguzi.

Maonesho ya kumi ya kibiashara ya kimataifa ya Zanzibar yalifanyika katika viwanja vilivyopo eneo la Fumba Dimani, Mkoa wa Mjini Magharibi kisiwani Unguja na yameshirikisha taasisi 500 zikiwemo za serikali, sekta binafsi, wafanyabiashara wakubwa na wadogo na wajasiriamali kutoka nje ya Tanzania na ndani ya Tanzania.

Kaulimbiu ya maonesho hayo ilikuwa **"Biashara Mtandao kwa Maendeleo ya Biashara na Uwekezaji".**

# TEMBELEENI TOVUTI NA MITANDAO YA KIJAMII YA TUME



***Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bw.Kailima, R. K, tarehe 30 Januari, 2024 ametembelea banda la Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma kwa siku saba kuanzia tarehe 24 hadi 30 Januari, 2024.***

**Na Mwandishi Wetu**

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Kailima, R. K amewaomba wananchi kutembelea mara kwa mara Tovuti na Kurasa za Mitandao ya Kijamii ya Tume ili kupata elimu ya mpiga kura.

Akizungumza baada ya kutembelea banda la Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika kuanzia tarehe 24 hadi 30 Januari, 2024 katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma, Bw. Kailima amesisitiza umuhimu wa wananchi kutembelea Tovuti na Kurasa za mitandao ya kijamii ya Tume ili kupata taarifa sahihi kuhusu mambo mbalimbali yanayoihusu Tume.

Amesema pamoja na majukumu mengine, Tume ina jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura ambapo wananchi wanapaswa kutumia fursa ya maonesho kama ya Wiki ya Sheria na mengine ambayo Tume inashiriki kwa ajili ya kupata ufafanuzi mzuri ili kuepuka upotoshaji kuhusu majukumu ya Tume ikiwa ni pamoja na jukumu la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwaka 2025.

"Tunawakaribisha wananchi kutembelea tovuti yetu na mitandao yetu ya kijamii ili kupata taarifa sahihi na kuepuka upotoshaji," amesisitiza Bw. Kailima na kuongeza:

"Mwakani, Mungu akitujaalia, tutaingia katika uchaguzi. Hivyo, tunawakaribisha wananchi kutembelea banda hili ili kupata taarifa mbalimbali. Njoo uulize maswali yako na upate ufafanuzi mzuri kuhusu mambo yanayohusu uboreshaji na uchaguzi mkuu".

Bw. Kailima ameongeza kuwa eneo hili ni zuri kwa wananchi kupata ufahamu wa lini uboreshaji utaanza, taratibu za uboreshaji na mambo mengine yanayohusu uchaguzi.

"Mathalani, kwa sasa tuna software (programu) inayoruhusu wale walioandikishwa kwenye daftari kuboresha taarifa zao kupitia simu. Hivyo, niwaombe wananchi watembelee banda la Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kupata taarifa mbalimbali zilizo sahihi," amesema.

Viongozi wengine wa Tume waliotembelea Banda la Tume katika maonesho ya Wiki ya Sheria ni pamoja na Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Jaji (Rufaa), Mhe. Jacobs Mwambegele, Makamu Mwenyekiti wa Tume Jaji wa Rufaa (Mstaafu), Mhe. Mbarouk Salim Mbarouk na Wajumbe wote wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Baada ya kumalizika kwa maonesho hayo, Mkurugenzi Msaidizi (Habari) wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bi. Leilla Muhaji, alipokea Cheti cha Ushiriki kilichotolewa na Mahakama kutambua ushiriki wa Tume kwenye maonesho hayo. Maonesho hayo yaliwashirikisha watumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi chini ya uongozi wa Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga Kura, Bi. Giveness Aswile.

Kilele cha Maonesho ya Wiki ya Sheria kilifanyika tarehe 01 Februari, 2024 katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hafla hiyo ilihudhuriwa na Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Jaji (Rufaa), Mhe. Jacobs Mwambegele na Mjumbe wa Tume Jaji (Rufaa), Mhe. Mwanaisha Kwariko.



***Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Tume, Mhe. Jaji wa Rufaa (Mstaafu), Mbarouk Salim Mbarouk, tarehe 29 Januari, 2024 wametembelea banda la Tume kwenye maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma kwa siku saba kuanzia tarehe 24 hadi 30 Januari, 2024.***

# NEC YATEUA MADIWANI WANAWAKE WATANO WA VITI MAALUM

**Na Mwandishi Wetu**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeteua Madiwani Wanawake watano wa Viti Maalum kujaza nafasi zilizokuwa wazi za Madiwani katika Halmashauri tano za Tanzania Bara.

Taarifa kwa umma iliyotolewa na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Kailima, R. K, imesema kwamba Tume imefanya uteuzi huo kwenye kikao chake cha tarehe 30 Januari, 2024.

"Uteuzi huu umefanyika baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, ambaye kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, aliitaarifu Tume ya Taifa ya Uchaguzi uwepo wa nafasi hizo wazi za Madiwani wanawake wa Viti Maalum," imesema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo imewataja walioteuliwa kuwa ni pamoja na Bi. Mecha Goodluck Matile ambaye ameteuliwa kuwa Diwani wa Viti Maalum katika Halmashauri ya Jiji la Tanga, Bi. Joyce Milembe Aenda ambaye ameteuliwa kuwa Diwani wa Viti Maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe na Bi. Sharifa Hassan Magalagala anayekuwa Diwani wa Viti Maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.

Wengine ni Bi. Clementina Daudi Mateja ambaye ameteuliwa kuwa Diwani wa Viti Maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa na Bi. Mariam Abdi Galu ambaye anakuwa Diwani wa Viti Maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.

## MATUKIO KATIKA PICHA



*Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele (kulia) akishiriki Matembezi ya ufunguzi wa Wiki ya Sheria Kitaifa Mkoani Dodoma Januari 27,2024. Matembezi hayo yaliongozwa na Spika wa Bunge, Mhe. Dkt. Tulia Ackson. Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yalianza Januari 24,2024 na yalifikia tamati Februari 1, mwaka huu.*



*Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiwa Bungeni jijini Dodoma. Bunge limepitisha Miswada miwili ya Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi mwaka 2023 na Mswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani mwaka 2023.*




*Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Kailima, R. K, akisaini kitabu cha wageni wakati alipotembelea banda la Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma kwa siku saba kuanzia tarehe 24 hadi 30 Januari, 2024.*



*Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Mhe. Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele (katikati) akiongoza kikao cha Tume jijini Dodoma ambapo pamoja na mambo mengine kiliteua madiwani watano wa viti Maalum. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Tume, Mhe. Jaji (Rufaa) Mstaafu, Mbarouk Salim Mbarouk na kulia ni Katibu wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Kailima, R. K.*

# WATUMISHI NEC WAITIKIA WITO WA KUFANYA MAZOEZI




*Timu ya Kamba wanaume kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wakivuta kamba dhidi ya Timu kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii katika Michezo inayohusisha Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) ambayo kwa mwaka 2023 ilifanyika mkoani Iringa mwezi Oktoba.*

**Na Mwandishi Wetu**

Wanamichezo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) katika kutekeleza wito unaotolewa mara kwa mara na viongozi wakuu wa serikali na wataalamu wa afya wameanza kujifua kwa kufanya mazoezi ya viungo mara nne kwa wiki.

Katibu wa Klabu ya Michezo ya NEC, Bw. Edward Kijanjali amesema kuwa kuanzia tarehe 05 Februari, 2024, wanamichezo hao wamekuwa wakikutana mara nne kwa wiki baada ya saa za kazi kwa ajili ya kufanya mazoezi ili kuweka afya zao zikae vizuri.

Amesema kuwa mazoezi hayo ambayo hufanyika kuanzia jumatatu hadi alhamis pamoja na kulenga kuweka afya sawa za watumishi wanaopenda michezo lakini pia ni katika kuitikia wito uliotolewa na viongozi wakuu wa serikali wakati wa ufunguzi wa Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI).

"Viongozi wetu wakuu wa serikali ambao ni Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu wakati wa ufunguzi wa SHIMIWI wamesisitiza kwa nyakati tofauti juu ya umuhimu wa watumishi wa umma kufanya mazoezi walau siku moja kwa wiki," amesema Bw. Kijanjali.

Ameongeza kuwa hata Mkurugenzi wa Uchaguzi amekuwa akitoa msisitizo kwa watumishi kuhusu kufanya mazoezi kwa ajili ya kuimarisha afya zao, hivyo klabu yake inatekeleza maagizo hayo kwa vitendo.

Bw. Kijanjali amewasihi watumishi wa NEC wanaopenda michezo kushiriki katika kufanya mazoezi kwani mbali na kuimarisha afya ya akili na mwili, mazoezi yanasaidia kujenga ushirikiano na umoja baina ya watumishi wa umma.

Mbali ya kufanya mazoezi ya viungo, klabu ya michezo ya NEC inajiandaa kushiriki kwenye Michezo ya Bonanza na Mashindano mengine yakiwemo SHIMIWI katika michezo ya kamba, mpira wa miguu, netiboli, riadha na michezo ya jadi.

***"Viongozi wetu wakuu wa serikali ambao ni Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu wakati wa ufunguzi wa SHIMIWI wamesisitiza kwa nyakati tofauti juu ya umuhimu wa watumishi wa umma kufanya mazoezi walau siku moja kwa wiki," amesema Bw. Kijanjali.***




**Tume ya Taifa ya Uchaguzi**
**Makao Makuu Dodoma,**
**5 Barabara ya Uchaguzi,**
**41107 Njedengwa,**
**Uchaguzi House,**
**Anuani: S.L.P 358, Dodoma**
**Namba ya simu: +255 26 2962345-8**
**Nukushi: +255 26 2962348**
**Barua pepe: Uchaguzi@nec.go.tz**

www.nec.go.tz tumeyauchaguzi_tanzania

Tume ya Uchaguzi-TZ Tume ya Uchaguzi-tz NEC online TV